BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2018

# KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2018

# KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA ........ 1

2.1 Sehemu A: Sarufi ........ 2

2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi ........ 27

2.3 Sehemu C: Ushairi ........ 41

2.4 Sehemu D: Utungaji ........ 50

2.5 Sehemu E: Ufahamu ........ 53

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI ........ 62

4.0 HITIMISHO ........ 63

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ........ 64

KIAMBATISHO A ........ 65

KIAMBATISHO B ........ **Error! Bookmark not defined.**

## DIBAJI

Taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Kiswahili mwaka 2018, imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi, watunga sera, wathibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu. Aidha, taarifa hii inaonesha jinsi mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji umeweza au kushindwa kumwezesha mwanafunzi kupata maarifa stahiki kwa kipindi cha miaka saba.

Sambamba na hayo, taarifa hii imechambua sababu mbalimbali zilizochangia baadhi ya watahiniwa kufaulu au kushindwa kujibu maswali kwa usahihi. Mathalan, baadhi ya sababu za kufaulu ni kuelewa matakwa ya swali pamoja na mada mbalimbali katika somo la Kiswahili. Aidha walishindwa kuelewa maana za msamiati, matakwa ya swali na kukosa maarifa kuhusu kanuni za lugha katika kuunda sentensi zenye muundo sahihi kisarufi. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila swali umeainishwa katika uchambuzi huu kwa kutumia maelezo, jedwali na vielelezo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wasimamizi wa elimu kubuni mbinu zitakazozidi kuimarisha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji ili kukabiliana na changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi ipasavyo, wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi watapata ujuzi na maarifa yanayotakiwa hivyo, kuwawezesha kukabiliana na changamoto mbalimbali katika mazingira yao baada ya Kumaliza Elimu ya Msingi.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki kuandaa taarifa hii wakiwemo Maafisa Mitihani, Wataalam wa TEHAMA na Wataalam Maalum wa Elimu walioshiriki katika uchambuzi na uandishi wa taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa hii ili kutoa mrejesho kuhusu jinsi ambavyo watahiniwa wamejibu maswali katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi katika somo la Kiswahili. Mtihani huu ulikuwa, na maswali **arobaini na tano** (**45)** ambapo maswali **arobaini (40)** ni ya kuchagua jibu sahihi na kila swali lilikuwa na alama **moja (01).** Maswali hayo yamegawanywa katika sehemu **nne (04)** kama ifuatavyo: Sehemu A: Sarufi; B: Lugha ya Kifasihi; C: Ushairi na D: Utungaji. Aidha, mtihani huu ulikuwa, na maswali **matano (05)** ya kujieleza kutoka sehemu E: Ufahamu ambayo yalikuwa na alama **mbili (02)** kwa kila swali. Jumla ya watahiniwa **957,904** walisajiliwa kufanya mtihani wa **PSLE 2018** somo la Kiswahili na waliofanya mtihani walikuwa **944,110**. Watahiniwa waliofaulu mtihani huu ni **805,685** sawa na asilimia **85.42**. Hata hivyo, uchambuzi wa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa haukufanyika kwa watahiniwa **6,424** waliofanya mtihani wa marudio.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umefanyika kwa kuainisha maswali yote ya mtihani ambayo yalikuwa ya kuchagua na kujieleza kwa kuangalia majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kila swali. Idadi na asilimia ya watahiniwa waliochagua kila chaguo, imeoneshwa kwa maelezo, jedwali na kielelezo. Rangi mbalimbali zimetumika kuonesha asilimia ya watahiniwa walioweza kujibu kila swali ambapo rangi ya njano imetumika kuwakilisha kiwango cha wastani cha kufaulu yaani asilimia **40 – 59.** Aidha, rangi ya kijani imetumika kuwakilisha kiwango kizuri cha kufaulu yaani asilimia **60 – 100**. Hata hivyo rangi nyekundu inayowakilisha kiwango hafifu cha kufaulu yaani **0 – 39** haikuweza kuoneshwa kwa mwaka 2018 kwa kuwa, hakuna watahiniwa waliopata

daraja hilo. Alama * imetumika katika jedwali na vielelezo kuonesha jibu sahihi lililotakiwa kwa kila swali. Vilevile, watahiniwa ambao yumkini wamechagua jibu zaidi ya moja au hawakufanya chaguo lolote wameoneshwa kwa neno "mengine".

## 2.1 Sehemu A: Sarufi

**Swali la 1:** Neno lipi kati ya maneno yafuatayo lina maana sawa na shari?

A Ubunifu

B Umaarufu

C Uzembe

D Ugomvi

E Uzushi

**Jedwali 2.1: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 134,417 | 127,287 | 68,623 | 498,908 | 103,833 | 4,847 |
| Asilimia ya watahiniwa | 14.33 | 13.57 | 7.32 | 53.19 | 11.07 | 0.52 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati wa Kiswahili. **Jedwali 2.1** linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 498,908 sawa na asilimia 53.19 waliweza kuchagua jibu sahihi D *Ugomvi.*

Watahiniwa 437,474 sawa na asilimia 46.3 walishindwa kubaini kisawe cha neno "shari" hivyo, wakachagua vipotoshi A *Ubunifu*, B *Umaarufu,* C *Uzembe* na E *Uzushi.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Ubunifu*, walishindwa kuelewa maana ya neno hilo ambalo si kisawe cha neno *shari* bali ni hali ya utengenezaji wa kitu

kwa mara ya kwanza. Aidha, waliochagua B *Umaarufu* ambayo ina maanisha hali ya kujulikana sana hawakuelewa dhana ya kisawe kuwa ni neno lenye maana sawa. Waliochagua chaguo C *Uzembe*, walikosa maarifa kuwa neno hilo ni hali ya kufanya kitu bila ya umakini na halilandani na neno shari na watahiniwa waliochagua chaguo E *Uzushi* ambayo maana yake ni hali ya kuzua mambo au maneno yasiyokuwa ya kweli walishindwa kuelewa kuwa maana ya maneno hayo siyo kisawe cha neno shari.

**Swali la 2:** Shida alivaa nguo za kijeshi wakati wa mkutano. Neno "za kijeshi" ni aina gani ya neno?

A Kivumishi

B Kielezi

C Kitenzi


D Kiwakilishi

E Nomino.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu ambapo watahiniwa 649,230 sawa na asilimia 69.23 walichagua vipotoshi B *Kielezi,* C *Kitenzi,* D *Kiwakilishi* na E *Nomino.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi B *Kielezi,* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuwa kielezi hakitoi taarifa juu ya nomino bali kinaelezea zaidi kuhusu kitenzi. Pia, uteuzi wa chaguo C *kitenzi* unatokana na watahiniwa kushindwa kuelewa kuwa, kitenzi ni neno linalotaja tendo. Vilevile, uteuzi wa D *Kiwakilishi* unaonesha kuwa watahiniwa hawakuelewa kuwa kiwakilishi ni maneno ambayo yanaweza kuchukuwa nafasi ya nomino katika sentensi. Aidha, uteuzi wa kipotoshi E *Nomino* ambayo hutaja majina ya watu, vitu au mahali unaonesha kuwa watahiniwa

hawakuwa na uelewa juu ya dhana ya kivumishi kuwa ni neno linalovumisha nomino kwa kueleza sifa yake ya ziada.

Watahiniwa wengine 285,492 sawa na asilimia 30.24 walichagua jibu sahihi A *Kivumishi.* Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa neno *za kijeshi* ni kivumishi cha a - unganifu kinachotoa taarifa zaidi juu ya nomino *nguo* katika sentensi. **Kielelezo 2.1** kinaonesha majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




**Kielelezo 2.1:** *takwimu za kiwango cha kufaulu ambapo 69.23% ya watahiniwa walishindwa kubaini kivumishi cha a-unganifu* “za kijeshi”.

**Swali la 3:** “Hicho ulichotaka sikupata lakini nimepata hiki.” Katika sentensi hii, maneno “hicho na hiki” ni aina gani ya maneno?

A Vivumishi

B Viwakilishi

C Vielezi

D Vitenzi

E Nomino.

**Jedwali 2.2: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 125,938 | 508,980 | 167,842 | 75,021 | 54,050 | 6,084 |
| Asilimia ya watahiniwa | 13.43 | 54.27 | 17.90 | 8.00 | 5.76 | 0.65 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa wa kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. **Jedwali 2.2** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 508,980 sawa na asilimia 54.27 waliweza kuchagua jibu sahihi B *Viwakilishi.* Uteuzi wa jibu hilo unaonesha kuwa watahiniwa waliweza kubaini kuwa neno hilo huchukua nafasi ya nomino katika sentensi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 422,851 sawa na asilimia 45.1 walichagua vipotoshi A *Vivumishi,* C *Vielezi,* D *Vitenzi* na E *Nomino.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Vivumishi* walishindwa kubaini kuwa, vivumishi huelezea zaidi nomino au kiwakilishi katika sentensi. Waliochagua C *Vielezi,* walishindwa kubaini kuwa, neno hilo hutumika kuelezea zaidi kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Vilevile, waliochagua kipotoshi D *Vitenzi* walishindwa kubaini kuwa ni maneno yanayoarifu juu ya ufanyikaji wa tendo na E *Nomino* ni neno linalotaja jina la mahali, mtu, kitu, hali au tendo na sio kiwakilishi. Uteuzi wa majibu hayo yasiyokuwa sahihi umetokana na watahiniwa hao kushindwa kuelewa dhana ya viwakilishi “hicho na hiki”kulingana na matakwa ya swali.

**Swali la 4:** Ni sentensi ipi iliyo sahihi kimuundo kati ya zifuatazo?

A Amenunua gari Mashaka

B Mashaka gari amenunua

C Amenunua Mashaka gari


D Mashaka amenunua gari

E Gari amenunua Mashaka.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lilikuwa linapima ujuzi wa mtahiniwa kutambua muundo sahihi wa sentensi. Kiwango cha

kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri zaidi kuliko maswali mengine ambapo watahiniwa 829,459 sawa na asilimia 88.44 waliweza kuchagua jibu sahihi D *Mashaka amenunua gari.* Hii inadhihirisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya muundo wa msingi wa sentensi katika lugha ya Kiswahili ambapo nomino huanza, kisha hufuata kitenzi na nomino (N+T+N).

Watahiniwa 104,457 sawa na asilimia 11.1 walishindwa kubaini muundo wa sentensi ulio sahihi katika swali. Watahiniwa hao walichagua kipotoshi A *Amenunua gari Mashaka* ambacho muundo wake (T+N+N) kwa matakwa ya swali hili hauko sahihi. Kipotoshi B *Mashaka gari amenunua,* pia kina muundo wa Nomino, Nomino na Kitenzi (N+N+T) ambao hauko sahihi kisarufi. Kipotoshi C *Amenunua Mashaka gari* sio mpangilio sahihi wa maneno katika sentensi kwani kitenzi hakiwezi kufuatiwa na nomino mbili (T+N+N). Aidha, kipotoshi E *Gari* amenunua Mashaka kina muundo sahihi kisarufi (N+T+N) lakini hakina maana kisarufi kulingana na muktadha wa swali. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo umeoneshwa katika **Kielelezo 2.2.**




**Kielelezo 2.2:** *kinaonesha kiwango cha kufaulu ambapo 88.44% ya watahiniwa waliweza kubaini muundo sahihi wa sentensi.*

**Swali la 5:** Maana nyingine ya neno ‘faraghani’ ni ipi kati ya hizi?

A Waziwazi

B Pembezoni

C Kivulini

D Mafichoni

E Hadharani

**Jedwali 2.3: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 97,815 | 41,692 | 128,471 | 478,795 | 183,609 | 7,533 |
| Asilimia ya watahiniwa | 10.43 | 4.45 | 13.70 | 51.05 | 19.58 | 0.80 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kufahamu maana ya msamiati mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kama kilivyooneshwa katika **Jedwali 2.3.** Watahiniwa 478,795 sawa na asilimia 51.05 walichagua jibu sahihi D *Mafichoni.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa kuwa neno *faraghani* ni mahala pa siri au pasipo watu.

Uchambuzi zaidi wa takwimu za kufaulu unaonesha kuwa, watahiniwa 451,587 sawa na asilimia 48.1 walichagua vipotoshi, A *Waziwazi,* B *Kivulini* C *Pembezoni* na E *Hadharani.* Watahiniwa hao walishindwa kuelewa maana ya kipotoshi A *waziwazi* ambacho maana yake ni kwa uwazi kinyume na faraghani, Waliochagua kipotoshi B *Kivulini* ambacho ni sehemu iliyofunikwa na kitu kinachozuia jua ingawa mahali hapo paweza kuwa pa wazi hawakuwa na uelewa wa dhana faraghani kuwa ni mahala pa siri. Pia waliochagua chaguo C *pembezoni* ambayo maana yake ni kandokando ya kitu fulani na E *hadharani* ambayo maana yake ni sawa na neno waziwazi hawakuwa na maarifa kuwa maneno hayo

siyo kisawe cha neno faraghani. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo umetokana na watahiniwa kushindwa kuelewa dhana ya maana nyingine ya neno au kisawe cha neno kuwa ni maana sawa ya neno moja na lingine ambapo kulingana na matakwa ya swali hili walitakiwa kueleza maana nyingine ya neno faraghani.

**Swali la 6:** Wingi wa sentensi, “Mbuzi wangu amepotea” ni upi?

A Mbuzi zetu zimepotea

B Mbuzi yetu zimepotea

C Mbuzi wetu wamepotea

D Mbuzi wetu zimepotea

E Mbuzi yetu wamepotea

**Jedwali 2.4: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 161,255 | 23,271 | 702,912 | 25,507 | 20,662 | 4,308 |
| Asilimia ya watahiniwa | 17.19 | 2.48 | 74.94 | 2.72 | 2.20 | 0.46 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua umbo la wingi katika sentensi. **Jedwali 2.4** linaonesha wa majibu ya watahiniwa katika swali hili. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 707,360 sawa na asilimia 74.94 waliweza kuchagua jibu sahihi C *Mbuzi wetu wamepotea.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya umoja na wingi katika lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya kwanza yu-a-wa.

Watahiniwa 232,452 sawa na asilimia 24.6 walichagua kipotoshi A *Mbuzi zetu zimepotea,* B *Mbuzi yetu zimepotea,* D *Mbuzi wetu zimepotea* na E *Mbuzi yetu wamepotea.* Watahiniwa waliochagua

vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa juu ya dhana ya upatanisho wa kisarufi katika ngeli ya kwanza kuhusu mabadiliko ya sentensi za umoja kuwa wingi.

**Swali la 7:** "Wanafunzi kenda walikwenda ziara nchini Kenya." Neno 'walikwenda' ni aina gani ya neno?

A Kiwakilishi

B Kivumishi

C Kielezi


D Kitenzi

E Nomino

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu ambapo watahiniwa 509,418 sawa na asilimia 54.0 walishindwa kuchagua jibu sahihi. Watahiniwa hao hawakuelewa aina za maneno ambapo walichagua vipotoshi A *Kivumishi,* B *Kiwakilishi,* C *Kielezi* na E *Nomino*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Kivumishi* walishindwa kuelewa kuwa neno *walikwenda* haliwezi kuwa kivumishi kwa kuwa, limerejelea tendo yani kitendo cha kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Waliochagua kipotoshi B *Kiwakilishi,* hawakuelewa kuwa neno hilo haliwakilishi nomino. Hali kadhalika kipotoshi C *Kielezi* ni neno linaloeleza jinsi tendo linavyofanyika, na haliwezi kuwa kitenzi. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi E *Nomino* hawakuelewa dhana ya kitenzi kwa kuwa, nomino ni maneno yanayotaja jina la kitu, vitu, mtu, watu na mahali ilhali neno walikwenda halitaji majina.

Jumla ya watahiniwa 427,893 sawa na asilimia 45.34 waliweza kuchagua jibu sahihi D *Kitenzi.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya kitenzi kuwa, ni neno

linaloonesha hali ya utendaji au kutenda jambo. Majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo yamefafanuliwa katika **Kielelezo 2.3.**




**Kielelezo 2.3:** *kinaonesha kiwango cha kufaulu ambapo 45.34% ya watahiniwa waliweza kubaini aina ya neno kama lilivyotumika katika sentensi.*

**Swali la 8:** Ashura anacheza mpira wa miguu vizuri. Katika sentensi hii, neno lipi limetumika kama kielezi?

A Anacheza

B Mpira

C Vizuri


D Ashura

E Wa miguu.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili ni cha wastani ambapo watahiniwa 500,012 sawa na asilimia 52.94 waliweza kuchagua jibu sahihi C *Vizuri.* Watahiniwa hao waliweza

kubaini maana ya kielezi kuwa, ni neno linaloeleza namna au jinsi tendo linavyofanyika.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 438,565 sawa na asilimia 46.5 walichagua vipotoshi A *Anacheza,* B *Mpira,* D *Ashura* na E *wa miguu.* Kipotoshi A *Anacheza,* hakiwezi kutumika kama kielezi katika sentensi kwani hakitoi taarifa ya ziada juu ya tendo la kucheza. Kipotoshi B *Mpira na* D *Ashura* ni nomino na siyo kielezi. Aidha, waliochagua kipotoshi E *wa miguu* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo ni kivumishi cha a-unganifu kwani kinaeleza zaidi kuhusu nomino “mpira” na siyo kielezi. **Kelelezo 2.4** kinaonesha asilimia ya majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




**Kielelezo 2.4:***kinaonesha kiwango cha kufaulu ambapo 52.94% ya watahiniwa waliweza kubaini aina ya maneno kama yalivyotumika katika sentensi.*

**Swali la 9:** Mtu anayefasiri ana kwa ana mazungumzo katika lugha moja kwenda lugha nyingine huitwaje?

A Msuluhishi

B Mpatanishi

C Mkalimani

D Mfafanuzi

E Mhubiri.

**Jedwali 2.5: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 58,134 | 81,546 | 518,484 | 213,711 | 58,859 | 7,181 |
| Asilimia ya watahiniwa | 6.20 | 8.69 | 55.28 | 22.79 | 6.28 | 0.77 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. **Jedwali 2.5** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 518,484 sawa na asilimia 55.28 waliweza kuchagua jibu sahihi C *Mkalimani.* Watahiniwa waliochagua jibu hilo walikuwa na maarifa ya kutosha kubaini kuwa, mkalimani ni mtu anayefasiri ana kwa ana mazungumzo kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine.

Watahiniwa wengine 412,250 sawa na asilimia 44.0 walichagua kipotoshi A *Msuluhishi,* B *Mpatanishi,* D *Mfafanuzi* na E *Mhubiri mtawalia.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Msuluhishi* na B *Mpatanishi* walishindwa kuelewa kuwa maneno hayo yana maana kuwa, ni watu wanaotafuta suluhu baina ya watu waliohitilafiana na sio mtu anayefasiri ana kwa ana mazungumzo kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. Waliochagua chaguo D *Mfafanuzi* yaani mtu anayetoa maelezo ya kina juu ya jambo fulani, walishindwa kuelewa maana ya mkalimani. Vilevile waliochagua kipotoshi E *Mhubiri* hawakuelewa dhana ya mkalimani kwani *mhubiri* ni mtu ambaye hutangaza au kutoa mawaidha ya dini.

**Swali la 10: “**Sote tunafanya mtihani darasani.” Neno “darasani” limetumika kama aina gani ya neno**?**

A Kielezi

B Kivumishi


C Kitenzi

D Kiwakilishi

E Nomino

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 491,985 sawa na asilimia 52.46 waliweza kuchagua jibu sahihi A *Kielezi.* Uteuzi wa chaguo hilo umetokana na watahiniwa kuwa na uelewa wa maana ya kielezi kuwa, ni neno lenye kueleza zaidi kuhusu ufanyikaji wa tendo.

Uchambuzi zaidi wa takwimu za kufaulu unaonesha kuwa, watahiniwa 441,522 sawa na asilimia 46.8 walichagua vipotoshi B *Kivumishi,* C *Kitenzi,* D *Kiwakilishi* na E *Nomino.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi B *Kivumishi,* walishindwa kuelewa dhana ya kivumishi kuwa ni neno linalotoa ufafanuzi zaidi kuhusu nomino. Uteuzi wa kipotoshi C *Kitenzi,* umetokana na watahiniwa kukosa maarifa ya kutosha kuhusu kitenzi kuwa ni neno linalotaja tendo linalofanyika na si kielezi. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi D Kiwakilishi walishindwa kuelewa kuwa kiwakilishi huchukua nafasi ya jina na pia uchaguzi wa kipotoshi E *Nomino* unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa kuhusu dhana ya nomino kuwa ni neno linalotaja kitu, mtu na mahali tofauti na kielezi. K**ielelezo 2.5** kinafafanua majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.5**: kinaonesha *kiwango cha wastani cha kufaulu ambapo 52.46% ya watahiniwa waliweza kubaini aina ya neno kama lilivyotumika katika sentensi.*

**Swali la 11:** Baraka aliona ______________kuwa, miongoni mwa waliofaulu. Ni neno lipi linakamilisha sentensi hii kwa usahihi kati ya maneno yafuatayo?

A fadhili

B fahari

C fahiri

D fadhaa

E fadhila

**Jedwali 2.6: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 86,764 | 621,851 | 39,033 | 60,352 | 123,475 | 6,440 |
| Asilimia ya watahiniwa | 9.25 | 66.30 | 4.16 | 6.43 | 13.16 | 0.69 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. **Jedwali 2.6** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa

kila chaguo. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 625,361 sawa na asilimia 66.30 waliweza kuchagua jibu sahihi B *fahari.* Watahiniwa hao walielewa maana ya neno fahari kuwa, ni hali ya watu kujivunia mambo waliyofanya au kufanyiwa.

Hata hivyo, watahiniwa 312,306 sawa na asilimia 33.1 walichagua vipotoshi A *fadhili,* C *fahiri,* D *fadhaa* na E *fadhila*. Kipotoshi A *fadhili* hakikuwa sahihi kwa kuwa, neno fadhili humaanisha kutoa msaada wakati wa haja au shida. Kipotoshi C *fahiri* hakikuwa sahihi kwa kuwa, neno fahiri humaanisha kutazama kitu kwa kupenda. Vilevile, kipotoshi D *fadhaa* hakikuwa sahihi kwani humaanisha hangaiko la moyo. Hali kadhalika, kipotoshi E *fadhila* kina maana ya ukarimu. Kwa jumla uteuzi wa chaguo hizo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kuelewa maana ya neno fahari ili kukamilisha sentensi.

**Swali la 12:** Mwanamke yule alikaa_______________baada ya kufiwa na mume wake. Ni neno lipi linakamilisha sentensi hii kati ya maneno yafuatayo?

A eda

B heda

C arobaini

D fungate

E edaha.

**Jedwali 2.7: Idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 428,732 | 156,006 | 167,563 | 120,845 | 56,150 | 8,619 |
| Asilimia ya watahiniwa | 45.71 | 16.63 | 17.87 | 12.88 | 5.99 | 0.92 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Muhtasari wa majibu ya watahiniwa umeoneshwa katika **Jedwali 2.7** ambapo watahiniwa 125,141 sawa na asilimia 53.4 walichagua vipotoshi B *heda* C *arobaini* na D *fungate* na E *edaha.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi B *heda* hawakuwa na maarifa kwani walishindwa kuelewa neno hilo halina uhusiano na eda. Waliochagua C *arobaini* hawakuelewa kuwa neno hilo ni siku ya arobaini ambayo aghalabu hutumika katika taratibu za waumini wa dini ya kiisamu kuadhimisha kumbukumbu ya siku arobaini baada ya mtu kufariki na D *fungate* inamaanisha mda wa siku saba baada ya harusi ambazo maharusi hutumia kwa mapumziko. Aidha, walichagua kipotoshi E *edaha* ambacho maana yake ni sadaka au tambiko tofauti na maana ya *eda*.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 428,732 sawa na asilimia 45.7 walichagua jibu sahihi A *eda* linalomaanisha muda maalum anaokaa mwanamke wa Kiislamu bila ya kuolewa baada ya kufiwa au kuachika na mumewe. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kubaini dhana ya msamiati *eda* kama linavyotumiwa katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 13:** Kitenzi “piga” kikiwa katika kauli ya kutendeka kitakuwa, neno lipi kati ya maneno yafuatayo?

A Pigia

B Pigwa


C Pigika

D Pigiwa

E Pigana

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kubaini kauli mbalimbali za vitenzi katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 588,448 sawa na asilimia 62.74 walichagua jibu sahihi C *Pigika* ambayo ni kauli ya kutendeka*.* Watahiniwa hao waliweza kubaini tabia ya kitenzi kupokea viambishi tamati baada ya mzizi wa neno -pig- ili kunyambulisha vitenzi na kupata kauli mbalimbali.

Watahiniwa 343,501 sawa na asilimia 36.6 walichagua kipotoshi A *Pigia,* B *Pigwa,* D *Pigiwa na* E *Pigana.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi A Pigia hawakuwa na uelewa kuwa neno hilo lipo katika kauli ya kutendea na watahiniwa waliochagua chaguo B Pigwa walishindwa kufahamu kuwa neno hilo lipo katika kauli ya kutendwa. Watahiniwa wengine walichagua kipotoshi D Pigiwa ambayo ni kauli ya kutendewa hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya kauli ya kutendewa. waliochagua E pigana walikosa maarifa juu ya kauli ya kutendeka wakahusisha na kauli ya kutendeana. Kwa jumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kubaini viambishi vya kauli mbalimbali za vitenzi ambapo kiambishi -i-, huwakilisha kauli ya kutendea, kiambishi -w- huwakilisha kauli ya kutendwa, kiambishi -iw- huwakilisha kauli ya kutendewa, na kiambishi -an- kinawakilisha kauli ya kutendana. **Kielelezo 2.6** kinaonesha asilimia ya majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




**Kielelezo 2.6:***kinaonesha kiwango cha kufaulu ambapo 62.74% ya watahiniwa, waliweza kubaini kauli ya kutendeka.*

**Swali la 14:** "Wewe unasoma kwa bidii." Wingi wa sentensi hii ni upi?

A Sisi tunasoma kwa bidii

B Wale wanasoma kwa bidii

C Ninyi mnasoma kwa bidii

D Ninyi tunasoma kwa bidii

E Wao wanasoma kwa bidii.

**Jedwali 2.8: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 331,580 | 60,477 | 432,301 | 30,876 | 77,817 | 4,864 |
| Asilimia ya watahiniwa | 35.35 | 6.45 | 46.09 | 3.29 | 8.30 | 0.52 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa kutambua sentensi yenye umbo la wingi katika lugha ya Kiswahili. **Jedwali 2.8** linaonesha majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo ambapo watahiniwa 500,750 sawa na asilimia 53.4 walichagua kipotoshi A *Sisi tunasoma kwa bidii,* B *Wale wanasoma*

*kwa bidii,* D *Ninyi tunasoma kwa bidii* na E *Wao wanasoma kwa bidii.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Sisi tunasoma kwa bidii* hawakuwa na uelewa kuwa sisi ni kiwakilishi cha nafsi ya kwanza wingi wakati swali lipo katika nafsi ya pili umoja. B *Wale wanasoma kwa bidiii* ni sentensi iliyopo kwenye nafsi ya tatu wingi wakati swali lipo kwenye nafsi ya pili umoja.Kipotoshi D *Ninyi tunasoma kwa bidii* ni sentensi isiyokuwa na upatanisho wa kisarufi kwani kiambishi tu- ni kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya kwanza wingi wakati swali linataka wingi wa sentensi. Aidha, kipotoshi E *Wao wanasoma* kwa bidii ni sentensi ya nafsi ya tatu wingi wakati swali linahitaji nafsi ya pili wingi. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya viwakilishi nafsi katika lugha ya Kiswahili.

Uchambuzi zaidi wa takwimu za kufaulu unaonesha kuwa, watahiniwa 432,301 sawa na asilimia 46.1 walichagua jibu sahihi C *Ninyi mnasoma kwa bidii* ambayo ni sentensi ya nafsi ya pili wingi. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu viwakilishi nafsi katika lugha ya Kiswahili. Mathalan, waliweza kubaini kuwa, swali lipo katika nafsi ya pili umoja na kutoa jibu sahihi ambalo lipo katika nafsi ya pili wingi.

**Swali la 15:** “Wanafunzi wale ni hodari sana.” Neno “wale” ni aina gani ya neno?

A Kitenzi

B Kivumishi

C Kielezi

D Nomino

E Kiwakilishi.

**Jedwali 2.9: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 71,061 | 290,737 | 83,217 | 141,891 | 345,847 | 5,162 |
| Asilimia ya watahiniwa | 7.58 | 31.00 | 8.87 | 15.13 | 36.87 | 0.55 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili. **Jedwali 2.9** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu ambapo watahiniwa 642,016 sawa na asilimia 68.5 walichagua kipotoshi A *Kitenzi,* C *Nomino,* D *Kielezi na* E *Kiwakilishi*. Watahiniwa waliochagua A *Kitenzi* hawakuwa na uelewa kuwa kitenzi ni neno linaloarifu tendo linavyofanyika wakati neno *wale* ni kivumishi kinachovumisha nomino, Uteuzi wa C *nomino* unaonesha kuwa, watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya nomino kuwa ni maneno yanayotaja jina la vitu, watu na mahali hivyo, neno wale si nomino bali ni kivumishi. Watahiniwa waliochagua D *Kielezi* hawakuwa na uelewa kuwa kielezi ni maneno yanayofafanua tendo lilivyofanyika na siyo kivumishi. Aidha, uteuzi wa kipotoshi E *Kiwakilishi* chenye maana ya maneno yanayowakilisha nomino katika sentensi, inaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina mbalimbali za maneno.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 290,737 sawa na asilimia 31.0 waliweza kuchagua jibu sahihi B *Kivumishi* ambalo ni neno linalotoa maelezo zaidi kuhusu nomino. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya aina za maneno hususan vivumishi katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 16:** “Wasichana saba wamechaguliwa kujiunga na kozi ya uhandisi.” Neno “na” ni aina gani ya neno?

A Kitenzi

B Nomino


C Kiwakilishi

D Kielezi

E Kiunganishi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kutambua aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 678,768 sawa na asilimia 72.37 walichagua jibu sahihi E *Kiunganishi*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa kuhusu dhana ya kiunganishi kuwa, ni neno linalounganisha maneno au sentensi.

Aidha, watahiniwa 253,507 sawa na asilimia 27.0 walichagua vipotoshi A *kitenzi,* B *Nomino,* C *Kiwakilishi* na D *Kielezi.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Kitenzi* chenye maana ya neno linaloarifu kuhusu ufanyikaji wa tendo hawakuwa na maarifa juu ya dhana ya kiunganishi kuwa hakiwezi kuelezea tendo bali hutumika kuunganisha neno na maneno mengine. Kipotoshi B *Nomino* inaonesha watahiniwa hawakuwa na uelewa kuhusu dhana ya nomino kuwa ni maneno yanayotaja jina la kitu, vitu, watu na mahali. Vile vile kipotoshi C *Kiwakilishi* siyo kiunganishi kwani ni maneno yanayowakilisha nomino na chaguo D *Kielezi* hawakuwa na uelewa kuwa kielezi ni maneno yanayofafanua tendo lilivyofanyika na siyo kiunganishi. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo umeoneshwa katika **Kielelezo 2.7.**




**Kielelezo 2.7:** *kinaonesha kiwango cha kufaulu ambapo 72.37% ya watahiniwa waliweza kubaini aina ya neno kulingana na matakwa ya swali.*

**Swali la 17:** Ni neno lipi lina maana sawa na hali ya kumzonga mtu kwa maneno makali kwa lengo la kumkasirisha?

A Kumhukumu

B Kumwinda

C Kumwadhibu

D Kumsakama

E Kumzomea

**Jedwali 2.10: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 106,284 | 54,045 | 93,161 | 453,219 | 223,239 | 7,967 |
| Asilimia ya watahiniwa | 11.33 | 5.76 | 9.93 | 48.32 | 23.80 | 0.85 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana sawa ya maneno (kisawe) katika sentensi. **Jedwali 2.10** ni majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 476,729 sawa na asilimia 50.8 walichagua kipotoshi A *Kumhukumu,* B *Kumwinda,* C *Kumwadhibu* na E *Kumzomea* mtawalia. Kipotoshi A *Kumhukumu* kina maana ya kutoa uamuzi

kwenye kesi ambapo maana hii inakinzana na matakwa ya swali. Watahiniwa waliochagua chaguo B *Kumwinda* kina maana ya kuvizia mnyama msituni kwa kumsaka na kumpiga kwa silaha tofauti na mahitaji ya swali kwani swali linamzungumzia binadamu na sio mnyama anayewindwa. Uteuzi wa kipotoshi C *Kumwadhibu* kina maana ya kumtesa mtu au kumtaabisha au kutoza mtu faini kwa makosa aliyofanya ambapo ni tofauti na matakwa ya swali. Aidha, kipotoshi E *Kumzomea* kina maana ya kutoa sauti kwa ajili ya kudhihaki au kudharau mtu. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na uelewa wa maana ya maneno hayo na kushindwa kueleza kisawe cha maana ya maneno “hali ya kumzonga mtu kwa maneno makali kwa lengo la kumkasirisha.

Watahiniwa 453,219 sawa na asilimia 48.3 walichagua jibu sahihi D *Kumsakama* ambalo ni kisawe cha hali ya kumzonga mtu kwa maneno makali ili kumkasirisha au kumkosesha raha. Uteuzi wa jibu sahihi unaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na uelewe wa maana mbalimbali za msamiati katika lugha ya Kiswahili

**Swali la 18:** Katika vitenzi “sitafyeka” na “hupendi” ni silabi zipi zinazoonesha ukanushi?

A ta na hu

B ta na pe

C ka na ndi


D si na hu

E fye na pe

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lilikuwa linapima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua silabi za ukanushi katika sentensi za lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali

hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 570,130 sawa na asilimia 60.79 walichagua jibu sahihi D *si na hu* ambazo ni silabi za ukanushi katika neno “sitafyeka “na “hupendi”.

Hata hivyo, watahiniwa 360,500 sawa na asilimia 38.4 walichagua vipotoshi A *ta na hu,* B *ta na pe,* C *ka na ndi* na E *fye na pe.* Kipotoshi A *ta na hu* kinafafanua kimakosa dhana ya ukanushi kwani, *ta* ni silabi ya njeo katika neno *sitafyeka* na siyo silabi kanushi japokuwa katika neno *hupendi* “*hu”* ni silabi kanushi. Kipotoshi B *ta na pe* siyo silabi za ukanushi kwani “*ta”* ni njeo ya wakati ujao katika kitenzi “sitafyeka” na “*pe”* ni silabi ya pili inayounda mzizi “pend” Kipotoshi C *ka na ndi*, ni silabi za mwisho katika maneno “sitafyeka na “hupendi” ambazo si za ukanushi. *Aidha,* kipotoshi E, *fye na pe*, ni silabi zinazojenga mzizi wa neno na siyo za ukanushi. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo umeoneshwa katika **Kielelezo 2.8.**




**Kielelezo 2.8:** *kinaonesha kiwango cha kufaulu ambapo 60.79% ya watahiniwa waliweza kubaini silabi za ukanushi “si na hu” katika swali.*

**Swali la 19:** Neno lipi kati ya haya yafuatayo halilandani na mengine?

A Cheka

B Tabasamu

C Furaha

D Sherehe

E Shere.

**Jedwali 2.11: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 32,897 | 50,913 | 34,769 | 145,848 | 666,410 | 7,078 |
| Asilimia ya watahiniwa | 3.51 | 5.43 | 3.71 | 15.55 | 71.05 | 0.75 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa kuhusu maana ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. **Jedwali 2.11** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 666,410 sawa na asilimia 71.05 walichagua jibu sahihi E *Shere* ambalo lina maana ya mzaha wa kumfanya mtu aonekane mjinga. Watahiniwa hao walielewa maana ya neno "shere" inatofautiana na maana za maneno katika machaguo mengine.

Jumla ya watahiniwa 264,427 sawa na asilimia 28.2 walichagua vipotoshi A *Cheka,* B *Tabasamu,* C *Furaha* na D *Sherehe.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi *cheka, tabasamu, furaha* vyenye dhana inayolandana yaani uchangamfu walichanganya dhana ya vipotoshi hivyo na neno *shere* kwa kudhani kuwa ni kifupi cha *sherehe* lakini isiyofanana na maana ya shere. Kipotoshi sherehe kina maana ya jambo la kufurahia yaani shamrashara ambalo pia halina maana sawa na "shere".

**Swali la 20:** “Mnyama huyu anafanana na ng’ombe.” Wingi wa sentensi hii ni upi?

A Wanyama anayefanana na ng’ombe

B Mnyama anayefanana na mang’ombe

C Wanyama hawa wanafanana na ng’ombe

D Wanyama wanaofanana na mang’ombe

E Mnyama wanaofanana na ng’ombe.

**Jedwali 2.12: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 42,453 | 45,371 | 741,047 | 57,177 | 41,063 | 10,804 |
| Asilimia ya watahiniwa | 4.53 | 4.84 | 79.01 | 6.10 | 4.38 | 1.15 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa wa kutambua umbo la wingi katika sentensi za lugha ya Kiswahili. **Jedwali 2.12** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 741,047 sawa na asilimia 79.01 walichagua jibu sahihi C *Wanyama hawa wanafanana na ng’ombe.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya wingi kwa kuwa, waliweza kubaini mabadiliko ya ngeli ya kwanza umoja kuwa, wingi (yu- a-wa) kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi katika sentensi hiyo.

Watahiniwa 186,064 sawa na asilimia 19.8 walichagua kipotoshi A *Manyama anayefanana na ng’ombe,* B *Mnyama anayefanana na mang’ombe,* D *Wanyama wanaofanana na mang’ombe* na E *Mnyama wanaofanana na ng’ombe.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kubaini umoja na wingi wa sentensi hususan ngeli ya yu-a-wa.

## 2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi

**Swali la 21:** Ni methali ipi kati ya zifuatazo inahimiza ushirikiano katika jamii?

A Chanda chema huvikwa pete

B Mchuma janga hula na wa kwao

C Umoja ni nguvu utengano ni dhaifu


D Mwenda pole hajikwai

E Wapishi wengi huharibu mchuzi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* na lilikuwa linapima ujuzi wa mtahiniwa katika kubaini maana na matumizi ya methali za Kiswahili. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri sana ambapo watahiniwa 786,923 sawa na asilimia 83.90 waliweza kuchagua jibu sahihi C *Umoja ni nguvu utengano ni dhaifu,* methali ambayo inahimiza ushirikiano katika jamii. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya methali ambayo inasisitiza ushirikiano.

Watahiniwa 145,022 sawa na asilimia 15.5 walichagua kipotoshi A *Chanda chema huvikwa pete,* B *Mchuma janga hula na wa kwao,* D *Mwenda pole hajikwai* na E *Wapishi wengi huharibu mchuzi.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Chanda chema huvikwa pete* hawakuwa na maarifa kwani maana ya methali hiyo ni kuwa mtu anayetenda mema katika jamii hupata baraka na haihimizi ushirikiano. Watahiniwa waliochagua, B *Mchuma janga hula na wa kwao* hawakuwa na maarifa kwani maana ya methali hiyo haihimizi ushirikiano bali inasisitiza kuwa mtu anayejitafutia matatizo kwa makusudi huwaathiri na anaoishi nao. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi D *Mwenda pole hajikwai* walishindwa kutambua kuwa methali hiyo haihimizi ushirikiano katika jamii

isipokuwa inaeleza kuwa mtu anayefanya kazi zake kwa umakini hufanikiwa. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi E *Wapishi wengi huharibu mchuzi* walishindwa kubaini kuwa dhana ya wapishi wengi sio ushirikiano bali ni kitendo cha kuwa na wasemaji wengi kwa jambo moja. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana za methali ambazo hutumika kwa ajili ya kutoa mafunzo yenye hekima kwa jamii. **Kielelezo 2.9** kinaonesha mtawanyo wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.9:** *kinaonesha kiwango cha kufaulu ambapo 83.90% ya watahiniwa waliweza kubaini maana ya methali "umoja ni nguvu utengano ni udhaifu".*

**Swali la 22:** "Watoto wa mfalme ni wepesi kujificha." Jibu la kitendawili hiki ni lipi?

A Macho

B Vifaranga

C Siafu

D Mvi

E Sungura

**Jedwali 2.13: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 767,775 | 57,854 | 45,363 | 28,068 | 32,866 | 5,989 |
| Asilimia ya watahiniwa | 81.86 | 6.17 | 4.84 | 2.99 | 3.50 | 0.64 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* na lilikuwa linapima ujuzi wa watahiniwa kubaini majibu ya vitendawili. **Jedwali 2.13** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Kiwango cha kufaulu kataka swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 767,775 sawa na asilimia 81.86 walichagua jibu sahihi A *macho* ambalo linategua kitendawili "*Watoto wa Mfalme ni wepesi kujificha",* hivyo walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo wa vitendawili

Watahiniwa 164,151 sawa na asilimia 17.5 walichagua kipotoshi B *Vifaranga,* C *Siafu,* D *Mvi* na E *Sungura kwa kukosa maarifa ya kutegua vitendawili.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi B *Vifaranga* walikuwa na dhana isiyo sahihi kwamba, kwa kuwa vifaranga huwa ni wepesi kukimbia na vinakumbatiwa na mama yao (kuku) hivyo wakalinganisha na kitendawili "*Watoto wa mfalme ni wepesi kujificha".* Watahiniwa waliochagua kipotoshi C *Siafu ambao* ni wadudu wadogo jamii ya chungu wanaokwenda pamoja katika makundi na huwa wanauma sana, D *Mvi ambazo* ni nywele nyeupe au za kijivu zinazomtoka mtu kichwani *na* E Sungura ambaye ni mnyama mdogo mwenye masikio marefu na mkia mfupi. Hivyo watahiniwa hawakuwa na maarifa kabisa ya kutegua vitendawili kwani hakuna uhusiano wa karibu kati ya maana za maneno hayo na kitendawili kilichotegwa.

**Swali la 23:** "Uzururaji umepigwa marufuku." Nahau 'umepigwa marufuku' ina maana gani?

A Umezoeleka

B Umepigwa winda

C Umepigwa konde

D Umekithiri


E Umekatazwa.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kutambua semi za Kiswahili. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 751,233 sawa na asilimia 80.10 walichagua chaguo sahihi E *Umekatazwa.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kubaini maana ya nahau *piga marufuku* kuwa, ni kumzuia mtu asitende jambo.

Watahiniwa 178,815 sawa na asilimia 19.1 walichagua vipotoshi A *Umezoeleka,* B *Umepigwa winda* C *Umepigwa konde* na D *Umekithiri.*

Watahiniwa hao hawakuwa na weledi wa kubaini dhana ya nahau "umepigwa marufuku" badala yake walichagua majibu yasiyo sahihi ambapo walichagua chaguo A *Umezoeleka* chenye maana ya kufanyika mara kwa mara na hivyo kufanya mtu au kitu kufahamika vyema ambapo haina uhusiano na matakwa ya swali. Watahiniwa wengine walichagua B *Umepigwa winda*, chenye maana ya shambulio la kuviziwa na mtu ili usiweze kufanya kitu ambacho pia sio dhana inayofanana na kukatazwa. Vilevile wapo watahiniwa waliokosea kwa kuchagua Kipotoshi C *umepigwa konde*, chenye maana ya kupigwa ngumi au sumbwi tofauti na matakwa ya swali. Aidha, kipotoshi D *Umekithiri* pia si jibu sahihi kwani maana yake ni kitu kuwa zaidi ya kingine au kupita mpaka. Kwa ujumla uteuzi wa

vipotoshi hivyo ambavyo havina uhusiano kabisa na nahau “umepigwa marufuku” unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa kuhusu semi za lugha ya Kiswahili hususan nahau **Kielelezo 2.10** kinaonesha mtawanyo wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.10:** *kinaonesha kiwango cha kufaulu ambapo 80.10% ya watahiniwa waliweza kubaini maana ya nahau “umepigwa marufuku”.*

**Swali la 24:** “Amenisamehe kwa moyo mweupe.” Nahau “moyo mweupe” ina maana ipi”?

A Bila kinyongo

B Kwa lazima

C Kwa shingo upande


D Kwa kusitasita

E Kwa kusuasua.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* na lililenga kupima maana na matuniai ya nahau. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili ni kizuri ambapo watahiniwa 803,550 sawa na asilimia 85.67 walichagua jibu sahihi A *Bila kinyongo* ambayo maana yake ni kutokuwa na vikwazo. Watahiniwa hao

walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya nahau *bila kinyongo* na kuweza kuihusisha na maana ya nahau *moyo mweupe.*

Aidha, watahiniwa 128,800 sawa na asilimia 13.7 walichagua kipotoshi B *kwa lazima* C *kwa shingo upande*, D *kwa kusitasita* na E *kwa kusuasua* watahiniwa hao walishindwa kutofautisha dhana ya nahau hizo ambazo zina maana sawa ambapo kipotoshi B *kwa lazima,* C *kwa shingo upande*, D *kwa kusitasita* na E *kwa kusuasua* vyote vina maana ya kufanya jambo bila hiari na havihusiani na dhana ya nahau “Amenisamehe kwa moyo mweupe”. **Kielelezo 2.11** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.11**:*kinaonesha kiwango cha kufaulu ambapo 85.67% ya watahiniwa waliweza kubaini maana ya nahau “moyo mweupe”.*

**Swali la 25:** “Mwenye nguvu ________________.” Neno lipi linakamilisha methali hii?

A Mfunge

B Usimkamate


C Mkimbie

D Usimpige

E Mpishe

Swali hili lilitoka katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* na lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa katika kutambua muundo na maana ya methali za Kiswahili. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 671,134 sawa na asilimia 71.56 waliweza kuchagua jibu sahihi E *Mpishe.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kwani waliweza kubaini maana ya neno "mpishe" kuwa lina maana ya kutoa nafasi ili mtu apite ili kukamilisha methali.

Hata hivyo, watahiniwa 257,392 sawa na asilimia 27.4 walichagua vipotoshi A *Mfunge,* B *Usimkamate,* C *Mkimbie* na D *Usimpige.* Uteuzi wa kipotoshi A *Mfunge* ulitokana na watahiniwa kuhusisha dhana ya kumfunga mtu kamba ambayo inakinzana na dhana ya neno *mpishe*. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi B *Usimkamate* na C *Mkimbie* walivutiwa na dhana kuwa, mtu mwenye nguvu inabidi umuepuke au umkalie mbali ili asikudhuru wakiihusisha kimakosa na neno *mpishe.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi D *Usimpige* walikuwa na dhana kuwa, usianzishe fujo au ugomvi na mtu mwenye nguvu kwani anaweza kutumia nguvu zake kukujeruhi ambapo waliihusianisha kimakosa na neno *mpishe* ili kukamilisha sentensi. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na weledi wa kutosha kukamilisha methali kulingana na matakwa ya swali. **Kielelezo 2.12** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.12:***kinaonesha takwimu za kiwango cha kufaulu ambapo 71.56% ya watahiniwa waliweza kukamilisha muundo wa methali "mwenye nguvu mpishe"*

**Swali la 26:** "Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu." Ni methali ipi inafanana na methali hii?

A Asiyesikia la mkuu huvunjika guu

B Asiye na mwana aeleke jiwe

C Asiye na bahati habahatishi

D Asiyejua kufa atazame kaburi

E Asiyekubali kushindwa si mshindani.

**Jedwali 2.14: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 779,860 | 43,504 | 27,703 | 35,458 | 46,173 | 5,217 |
| Asilimia ya watahiniwa | 83.15 | 4.64 | 2.95 | 3.78 | 4.92 | 0.56 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana ya methali za Kiswahili. **Jedwali 2.14** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Watahiniwa 779,860 sawa na asilimia 83.15 waliweza kuchagua jibu sahihi A *Asiyesikia la mkuu huvunjika guu* kwani walikuwa na maarifa yaliyowawezesha kuelewa methali inayofanana nayo. Methali hii ina maana kuwa,

mtu asiyefuata mafundisho ya wakubwa wake hupata matatizo makubwa maishani mwake sawa na methali isemwayo "*Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu".*

Watahiniwa 152,854 sawa na asilimia16.3 walichagua vipotoshi B *Asiye na mwana aeleke jiwe,* C *Asiye na bahati habahatishi,* D *Asiyejua kufa atazame kaburi* na E *Asiyekubali kushindwa si mshindani*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi B *Asiye na mwana aeleke jiwe* ambapo ni hali ya kukubaliana na hali halisi ya kutokuwa na kitu walishindwa kuelewa kuwa maana ya methali hiyo haifanani na methali asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu ambayo maana yake ni asiyefuata mafundisho ya wakubwa wake hupata matatizo makubwa maishani mwake. Aidha watahiniwa waliochagua C *Asiye na bahati habahatishi* kina chenye maana kuwa unaweza kutenda jambo fulani vizuri lakini usiambulie lolote au chochote walishindwa kuelewa kuwa maana ya methali hiyo siyo sawa na methali katika swali. Waliochagua kipotoshi D *Asiyejua kufa atazame kaburi* yenye maana kuwa tunapaswa kujifunza kutokana na makosa ya wenzetu kipotoshi E *Asiyekubali kushindwa si mshindani* inayomaanisha kuwa asiyekubali matokeo hasi katika maisha yake basi hafai kuigwa na watu wengine, walishindwa kuelewa maana ya methali hizo kuwa hazina uhusiano kabisa na matakwa ya swali

**Swali la 27:** “Haba na haba hujaza kibaba.” Methali hii inatoa funzo gani?

A Umuhimu wa kupima vitu

B Tunapaswa kujiwekea akiba


C Vitu hupimwa na kibaba tu

D Tunapaswa kupima vibaba

E Kibaba hujaza vitu.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* na ililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua funzo kutokana na methali za Kiswahili. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 691,170 sawa na asilimia 73.69 walichagua jibu sahihi B *Tunapaswa kujiwekea akiba* sawa na funzo linalopatikana katika methali "*Haba na haba hujaza kibaba".*

Uchambuzi zaidi wa takwimu za kufaulu unaonesha kuwa, watahiniwa 241,045 sawa na asilimia 25.7 walichagua kipotoshi A *Umuhimu wa kupima vitu,* C *Vitu hupimwa na kibaba tu,* D *Tunapaswa kupima vibaba* na E *Kibaba hujaza vitu.* Mafunzo ya vipotoshi hivyo havina uhusiano na jibu sahihi la funzo linalopatikana kutokana na methali *Haba na haba hujaza kibaba.* **Kielelezo 2.13** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo




**Kielelezo 2.13**: *kinaonesha takwimu za kiwango cha kufaulu ambapo 73.69% ya watahiniwa waliweza kubaini funzo linalotokana na methali "Haba na haba hujaza kibaba".*

**Swali la 28:** "Heri kufa macho kuliko _______________". Methali hii hukamilishwa na kifungu kipi cha maneno?

A Kujikwaa ulimi

B Kuumia moyo

C Kuzama majini


D Kufa moyo

E Kufa jicho moja

Swali hili lilitoka katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kukamilisha muundo wa methali katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 697,162 sawa na asilimia 74.33 walichagua D *Kufa moyo* ikiwa na maana ya kukata tamaa ambapo kinakamilisha methali kulingana na matakwa ya swali.

Uchambuzi zaidi wa takwimu za kufaulu unaonesha kuwa, watahiniwa 236,421 sawa na asilimia 25.2 walichagua vipotoshi A *Kujikwaa ulimi,* B *Kuumia moyo,* C *Kuzama majini* na E *Kufa jicho moja.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Kujikwaa ulimi* chenye maana ya kusema neno bila kukusudia, walivutiwa na dhana kuwa, *jicho ni bora kuliko ulimi.* Aidha, uteuzi B *Kuumia moyo* kuliwavutia kwa kuwa maana yake ni kutofurahishwa ambapo walihusisha na dhana kuliko kufa macho ni afadhali kuumia moyo. Waliochagua C *Kuzama majini* yenye maana ya kuingia ndani ya maji walihusisha na dhana kuwa ukiingia majini utakufa hivyo ni heri ufe jicho lakini uendelee kuwa hai. Vilevile watahiniwa waliochagua kipotoshi E *Kufa jicho moja* ambayo maana yake ni kupoteza uwezo wa jicho kuona, walikuwa na dhana kuwa heri nusu shari kuliko shari kamili. Kwa jumla, dhana za vipotoshi hivyo ni tofauti na dhana ya methali *Kufa moyo* hivyo, haviwezi kuwa vikamilisho vyake. **Kielelezo 2.14**

kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.14**: *kinaonesha kiwango cha kufaulu ambapo 74.33% ya watahiniwa waliweza kukamilisha muundo wa methali "Heri kufa macho kuliko kufa moyo"*

**Swali la 29:** "Maji yakimwagika hayazoleki."Methali hii ina maana gani kati ya zifuatazo?

A Ukitaka usizoe maji, usimwage

B Tuwe waangalifu katika kutenda jambo

C Tuwe waangalifu tunapobeba maji

D Maji yakimwagika hugeuka matope

E Jambo lililoharibika halitengenezeki.

**Jedwali 2.15: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 42,745 | 345,910 | 41,988 | 76,347 | 424,212 | 6,713 |
| Asilimia ya watahiniwa | 4.56 | 36.88 | 4.48 | 8.14 | 45.23 | 0.72 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana za methali za Kiswahili. **Jedwali 2.15** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa

kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 506,990 sawa na asilimia 54.1 walichagua vipotoshi A *Ukitaka usizoe maji, usimwage,* B *Tuwe waangalifu katika kutenda jambo,* C *Tuwe waangalifu tunapobeba maji na* D *Maji yakimwagika hugeuka matope*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa kubainii dhana ya methali "Maji yakimwagika hayazoleki" ambapo walichagua chaguo ambazo maana zake ni tofauti na jibu sahihi la swali. Kwa mfano, kipotoshi A *Ukitaka usizoe maji, usimwage* waliangalia maana yake katika umbo la nje (maana ya moja kwa moja) kuwa, ili usizoe maji basi usiyamwage, na waliochagua B *Tuwe waangalifu katika kutenda jambo,* maana yake ni unapofanya jambo lazima uwe mwangalifu ili usije kufanya makosa. Vile, vile watahiniwa waliochagua kipotoshi C *Tuwe waangalifu tunapobeba maji,* na D *Maji yakimwagika hugeuka matope* walizingatia maana ya nje kuwa, tuwe waangalifu tunapobeba ndoo ya maji kwa kuwa, maji yakimwagika huwa matope.

Aidha, watahiniwa 424,212 sawa na asilimia 45.23 walikuwa waliweza kuchagua jibu sahihi E *Jambo lililoharibika halitengenezeki, y*enye maana sawa na methali "Maji yakimwagika hayazoleki" Maana ya methali hiyo ni kuwa, mambo yaliyoharibika huwa yamekwisha haribika wala hayawezi kutengenezeka na hata kama ingewezekana hayawi kama awali. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya maana za methali.

**Swali la 30:** "Amani haiji ____________. Kifungu kipi cha maneno kinakamilisha methali hii kwa usahihi?

A Ila kwa mzozo mkubwa

B Ila kwa malumbano makali

C Bila kuwa, na imani

D Ila kwa ncha ya upanga

E Bila makubaliano

**Jedwali 2.16: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 50,354 | 62,898 | 315,169 | 275,896 | 225,092 | 8,506 |
| Asilimia ya watahiniwa | 5.37 | 6.71 | 33.60 | 29.42 | 24.00 | 0.91 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua kifungu cha maneno kinachokamilisha methali. **Jedwali 2.16** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili hakikuwa kizuri ambapo watahiniwa 653,513 sawa na asilimia 69.7 walichagua vipotoshi A *Ila kwa mzozo mkubwa* B *Ila kwa malumbano makali,* C *Bila kuwa, na imani* na E *bila makubaliano.* Watahiniwa waliochagua chaguao A *Ila kwa mzozo mkubwa* yenye kumaanisha hali ya kutoelewana na kubishana kwa sauti kubwa, hawakuelewa kuwa dhana hiyo inakinzana na maana ya kifungu cha maneno "Ila kwa ncha ya upanga" ambayo ni kikamilisho sahihi cha methali. Waliochagua B *Ila kwa malumbano makali* inayomaanisha majadiliano yanayotawaliwa na maswali na majibu baina ya washiriki, walikosa maarifa kuhusu maana ya malumbano wakahusisha dhana yake na kikamilisho cha methali. Waliochagua chaguo C *Bila kuwa na imani* ambayo ni bila kuwa na huruma walihusisha dhana ya amani na tendo la huruma na uteuzi E *bila makubaliano* ambayo ni bila mapatano walikosa maarifa ya kutofautisha dhana ya *ncha ya upanga* na *malumbano.* Kwa jumla, watahiniwa hao hawakuweza kuelewa dhana ya vifungu vya maneno ili kukamilisha methali.

Hata hivyo, watahiniwa 275,896 sawa na asilimia 29.42 waliweza kukamilisha methali kwa kuchagua jibu sahihi D *Ila kwa ncha ya upanga* jambo linaloonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya vifungu vya maneno. Aidha, waliweza kubaini dhana ya methali *amani haiji ila kwa ncha ya upanga* ambayo inahimiza watu wanaoonewa lazima wafanye jitihada za kuondoa uonevu.

## 2.3 Sehemu D: Ushairi

Watahiniwa walitakiwa kusoma shairi kisha wajibu maswali yanayotokana na shairi hilo. Lifuatalo ni shairi walilopewa watahiniwa.

Kazi ifanye kwa nia, itakupatia tija,
Ifanye kwa kupania, iwe kwako ni daraja,
Kazi ni kuibobea, ili ilete faraja,
Juhudi katika kazi, ni zawadi maridhawa.

Ni zawadi maridhawa, juhudi katika kazi,
Ifanye uwe mzawa, uonekane mzazi,
Uoneshe uelewa, nchini mwako azizi,
Tufanye kazi kwa dhati, itatupa manufaa.

Itatupa manufaa, tufanye kazi kwa dhati,
Tuoneshe yanofaa, kwa moyo ulo thabiti,
Pasiwe kizaa zaa, tusoweza kuthibiti,
Kazi ndio mhimili, popote utapokuwa,.

Popote utapokuwa,, kazi ndio mhimili,
Kama gari huendeshwa, vile inastahili,
Mafunzo uliyopewa, yawe kwako ni kivuli,
Kwako kazi ni muhimu, maisha kuendelea.

**Swali la 31:** Kichwa kinachofaa kwa shairi hili ni kipi kati ya vifuatavyo?

A Juhudi katika kazi

B Mafunzo ya kazi


C Kazi inayostahili

D Kazi inayofaa

E Changamoto za kazi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ushairi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua kichwa cha shairi alilolisoma. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 697,108 sawa na asilimia 74.33 walichagua jibu sahihi A *Juhudi katika kazi.* Watahiniwa waliochagua chaguo hilo walikuwa na maarifa kuwa, kichwa cha shairi kinatokana na mawazo makuu ambayo yanajirudia katika kila ubeti wa shairi.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 232,550 sawa na asilimia 24.8 walichagua vipotoshi B *Mafunzo ya kazi,* C *Kazi inayostahili,* D *Kazi inayofaa* na E *Changamoto za kazi.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi B *Mafunzo ya kazi* walivutiwa na dhana ya watu kujifunza kazi ambayo siyo jibu sahihi kwani shairi linahimiza wananchi wafanye kazi kwa bidii. Uchaguzi C *Kazi inayostahili,* ulisababishwa na watahiniwa kuvutiwa na ubeti wa nne unaosisitiza umuhimu wa kazi. Aidha, uteuzi D *Kazi inayofaa* ulitokana na watahiniwa kuhusisha ujumbe wa shairi na ubeti wa pili katika mstari wa mwisho "*Tufanye kazi kwa dhati, itatupa manufaa"* na ubeti wa tatu mstari wa kwanza "*Itatupa manufaa, tufanye kazi kwa bidii*". Hata hivyo, uchaguzi wa kipotoshi E *Changamoto za kazi* ulitokana na maana ya neno changamoto ambayo ni hamu ya kufanya kitu. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo hauendani na kichwa cha shairi kwani maneno hayo siyo wazo kuu la shairi. **Kielelezo 2.15** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.15**:*kinaonesha takwimu za kiwango cha kufaulu ambapo 74.33% ya watahiniwa waliweza kubaini kichwa cha shairi.*

**Swali la 32:** Mwandishi anasema "kazi ni kuibobea" ana maana gani?

A Kuipenda na kuithamini

B Kuleta faraja

C Kuijua na kuifanya ipasavyo


D Kuifanya kwa kutumia nguvu

E Kazi ndio muhimili.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ushairi* na lilikuwa linapima ujuzi wa mtahiniwa kubaini semi na matumizi yake kama ilivyotumika katika shairi. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa hafifu ambapo watahiniwa 583,126 sawa na asilimia 62.2 walichagua vipotoshi A *Kuipenda na kuithamini*, B *Kuleta faraja*, D *Kuifanya kwa kutumia nguvu* na E *Kazi ndio muhimili*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Kuipenda na kuithamini*, walivutiwa na maneno yaliyopo katika shairi ubeti wa kwanza *kazi ifanye kwa nia, itakupatia tija.* Uteuzi wa chaguo B *Kuleta faraja* umetokana na watahiniwa kuvutiwa na usemi *kazi ni kuibobea.* Aidha, watahiniwa

waliochagua kipotoshi D Kuifanya kwa kutumia nguvu walivutiwa na maneno kwenye ubeti wa kwanza mstari wa nne kuwa, *Juhudi katika kazi* na uteuzi wa kipotoshi E *Kazi ndio muhimili* ulitokana na neno *kazi ndio mhimili* kutoka mstari wa nne katika ubeti wa tatu. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu usemi usemao "kazi ni kuibobea" katika shairi.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 346,718 sawa na asilimia 36.97 walichagua jibu sahihi C *Kuijua na kuifanya ipasavyo.* Uchaguzi wa chaguo hilo unaonesha kuwa, watahiniwa hao walielewa maana ya usemi kuwa, *kazi ni kuibobea* maana yake ni kujishughulisha na jambo fulani kupita kiasi. **Kielelezo 2.16** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo




**Kielelezo 2.16:** *kinaonesha kiwango cha kufaulu ambapo 62.2% ya watahiniwa walishindwa kuelezea maana ya "kazi ni kuibobea".*

**Swali la 33:** Vina vya kati na mwisho katika ubeti wa pili ni vipi?

A wa na ju

B wa na u


C ti na i

D ti na a

E wa na zi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ushairi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 721,842 sawa na asilimia 76.96 waliweza kuchagua jibu sahihi E *wa na zi* ambazo ni silabi za mwisho katika kila kipande cha ubeti wa pili wa shairi. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo wa shairi.

Hata hivyo, watahiniwa 207,225 sawa na asilimia 22.1 walichagua vipotoshi A *wa na ju,* B *wa na u,* C *ti* na *i,* D *ti na a.* Watahiniwa hao walikosa maarifa juu ya dhana ya vina katika shairi kwani walichagua silabi ambazo zimetokea katika shairi kwenye nafasi ambazo haziwezi kuwa na sifa ya vina vya kati wala vya mwisho kwa mujibu wa kanuni za muundo wa shairi katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na uchaguzi wa vipotoshi hivyo, inathibitisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya vina vya kati na mwisho katika ubeti wa pili wa shairi. **Kielelezo 2.17** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.17:** *takwimu za kiwango cha kufaulu ambapo 76.96% ya watahiniwa waliweza kubaini vina vya kati na mwisho katika shairi.*

**Swali la 34:** Shairi hili linatoa funzo gani?

A Ni vema kuithibitisha kazi

B Kazi ni muhimu katika maisha

C Ni bora kuajiriwa


D Ni muhimu kupewa mafunzo

E Watu wafanye kazi ili wapate zawadi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ushairi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kubaini funzo kutokana na shairi. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 695,204 sawa na asilimia 74.12 walichagua jibu sahihi B *Kazi ni muhimu katika maisha.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha hivyo, waliweza kubaini kuwa msisitizo wa mistari ya mwisho katika kila ubeti ndio uliobeba umuhimu wa kazi. Kwa mfano ubeti wa pili "*Tufanye kazi kwa dhati, itatupa manufaa"*.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 234,687 sawa na asilimia 25.0 walishindwa kubaini funzo linalopatikana katika shairi kwa kukosa maarifa ya kubaini wazo kuu la shairi. Watahiniwa hao walichagua vipotoshi A *Ni vema kuithibitisha kazi,* C *Ni bora kuajiriwa,* D *Ni muhimu kupewa mafunzo na* E *Watu wafanye kazi ili wapate zawadi.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Ni vema kuithibitisha kazi* hawakuelewa kuwa, neno hilo halifafanui funzo la shairi kwani siyo neno lililosisitizwa katika kila ubeti. Vilevile waliochagua C *Ni bora kuajiriwa*, walihusianisha maneno ya ubeti wa kwanza mstari wa nne kuwa "juhudi katika kazi, ni zawadi maridhawa" kwamba mtu akiwa na juhudi katika kazi atapata zawadi. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi D *Ni muhimu kupewa mafunzo* walivutiwa na jibu hilo kutokana na ubeti wa nne mstari wa tatu usemao "Mafunzo uliyopewa, yawe kwako ni kivuli" ikiwa na maana kuwa mambo

mazuri uliyojifunza yawe msaada mkubwa katika maisha. Mwisho waliochagua E *Watu wafanye kazi ili wapate zawadi,* ikiwa na maana ukifanya kazi kwa bidii utapata tuzo kazini, walivutiwa na ubeti wa pili usemao “Ni zawadi maridhawa, juhudi katika kazi”. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha kutambua funzo lililotolewa katika shairi. **Kielelezo 2.18** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.18:** *kiwango cha kufaulu ambapo 74.12% ya watahiniwa waliweza kueleza funzo la shairi.*

**Swali la 35:** Neno “thabiti” katika shairi hili lina maana gani?

A Mkunjufu

B Mnyenyekevu

C Mweupe


D Madhubuti

E Mwepesi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ushairi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika

shairi. Kiwango cha kufaulu katika swali hili hakikuwa kizuri ambapo watahiniwa 735,980 sawa na asilimia 78.5 watahiniwa hao walichagua vipotoshi A *Mkunjufu*. B *Mnyenyekevu,* C na E *Mwepesi* Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Mkunjufu* hawakuwa na uelewa wa maana ya neno hilo kuwa ni kutokuwa na kinyongo ambayo inakinzana na maana ya *thabiti.* Aidha, watahiniwa waliochagua B *Mnyenyekevu,* hawakutambua kuwa neno hilo huonesha tabia ya unyenyekevu, uteuzi C *Mweupe* hawakuelewa kuwa ni kivumishi kinachobainisha rangi ya mnyama au mwangaza na si kiwakilishi cha dhana *thabiti* na E *Mwepesi* hawakuelewa kuwa ni kielezi cha hali ya ujazo. Hivyo, kutokana na maana za vipotoshi hivyo inadhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa yakutosha kubaini maana ya msamiati "thabiti" ambao unamaanisha msimamo madhubuti katika kufanya jambo kama ulivyotumika katika shairi.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 192,393 sawa na asilimia 20.51 waliweza kuchagua jibu sahihi D *Madhubuti* ikiwa na maana kitu chenye nguvu au uimara. Watahiniwa hao waliweza kuhusianisha msamiati *thabiti* na neno *madhubuti* ambalo linabeba maana ya msingi ya msamiati *thabiti* kama lilivyotumika katika shairi. **Kielelezo 2.19** kinaonesha asilimia ya majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




**Kielelezo 2.19:** *kiwango cha kufaulu ambapo 78.5% ya watahiniwa walishindwa kutoa maana ya neno thabiti.*

**Swali la 36:** Unafikiri mwandishi ana maana gani anaposema "mafunzo uliyopewa yawe kwako ni kivuli"

A Yasikuweke juani

B Yakuweke chini ya mti

C Yawe ndio ushahidi

D Yalete matukio

E Yawe ya mafanikio

**Jedwali 2.17: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 73,042 | 54,357 | 93,587 | 50,504 | 656,435 | 9,990 |
| Asilimia ya watahiniwa | 7.79 | 5.80 | 9.98 | 5.38 | 69.99 | 1.07 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ushairi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kubaini maana ya usemi katika shairi. **Jedwali 2.17** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 656,435 sawa na asilimia 69.99 walichagua jibu sahihi E *Yawe ya mafanikio.* Watahiniwa hao waliweza kueleza maana ya

usemi “mafunzo uliyopewa yawe kwako ni kivuli” ambapo neno “kivuli” limetumika kama ishara ya mahali pa kupumzika baada ya kufanya kazi fulani.

Hata hivyo, watahiniwa 271,490 sawa na asilimia 28.9 walichagua vipotoshi A *Yasikuweke juani*, B *Yakuweke chini* ya mti, C *Yawe ndio ushahidi* na D *Yalete matukio*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *Yasikuweke juani* hawakuwa na uelewa kuwa, kauli *mafunzo uliyopewa yawe kwako ni kivuli* maana yake ni *dira ya kufanikisha jambo*, tofauti na dhana ya yawe ya mafanikio. Aidha watahiniwa waliochagua kipotoshi B *Yakuweke chini ya mti*, walihusianisha dhana hiyo na neno kivuli kuwa kinapatikana chini ya mti. Kipotoshi C *Yawe ndio ushahidi*, watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki walishindwa kuhusianisha maana sahihi ya “mafunzo uliyopewa yawe kwako ni kivuli” Hata hivyo, watahiniwa waliochagua kipotoshi D *Yalete matukio* walishindwa kuelewa neno hilo lina maanisha kuwa, ni mafunzo uliyoyapata lazima yafanyiwe kazi ili yalete mafanikio si dhana sahihi kulingana na matakwa ya swali.

## 2.4 Sehemu D: Utungaji

Katika sehemu hii watahiniwa walipewa sentensi nne (4) zilizoandikwa bila mtiririko sahihi na walitakiwa wazipange sentensi hizo ili ziwe na mtiririko wenye mantiki kwa kuzipa herufi A, B, C na D.

**Jedwali .2.18 Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Swali | Jibu Sahihi | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa | Mengine (%) | Jibu E (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| **40** | A | 699,938 | 74.63 | 2.13 | 0.72 |
| **38** | B | 579,478 | 61.78 | 1.73 | 0.86 |
| **37** | C | 438,707 | 46.77 | 2.61 | 0.89 |
| **39** | D | 425,654 | 45.38 | 2.69 | 0.83 |

**Swali la 37:** Kwa mfano, wavulana walipofika umri wa kuoa iliwalazimu kujijengea nyumba za kuishi na kuwa na shamba la mazao ya chakula.

**Jedwali 2.19: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 51,908 | 106,046 | 438,707 | 308,468 | 24,449 | 8,337 |
| Asilimia ya watahiniwa | 5.53 | 11.31 | 46.77 | 32.89 | 2.61 | 0.89 |

**Swali la 38:** Elimu hiyo ilitolewa na walimu maalum wa jadi na ilihusisha sana vitendo.

**Jedwali 2.20: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 68,392 | 579,478 | 180,192 | 85,594 | 16,185 | 8,074 |
| Asilimia ya watahiniwa | 7.29 | 61.78 | 19.21 | 9.13 | 1.73 | 0.86 |

**Swali la 39:** Wakati wa ukoloni elimu hiyo ilipigwa vita na kuonekana kuwa, haifai hivyo ulileta mfumo mpya wa elimu.

**Jedwali 2.21: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 98,210 | 151,988 | 229,058 | 425,654 | 25,190 | 7,815 |
| Asilimia ya watahiniwa | 10.47 | 16.20 | 24.42 | 45.38 | 2.69 | 0.83 |

**Swali la 40:** Kabla ya kuja kwa wakoloni Waafrika walikuwa na mfumo wao wa elimu ya jadi.

**Jedwali 2.22: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 699,938 | 86,166 | 70,182 | 54,977 | 19,944 | 6,708 |
| Asilimia ya watahiniwa | 74.63 | 9.19 | 7.48 | 5.86 | 2.13 | 0.72 |

Sehemu hii ililenga kupima uwezo wa watahiniwa wa kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki. **Jedwali 2.18** linaonesha kuwa, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo idadi kubwa ya watahiniwa waliweza kupanga kwa usahihi sentensi ya kwanza hadi ya mwisho. Watahiniwa 699,938 sawa na asilimia 74.63 waliweza kupanga sentensi ya kwanza (Na. 40) kwa usahihi kwa kuandika herufi A. Vilevile, watahiniwa 579,478 sawa na asilimia 61.78 walipanga na kuandika sentensi ya pili (Na.38) kwa usahihi kwa kuandika herufi B. Hali kadhalika, watahiniwa 438,707 sawa na asilimia 46.77 waliweza kupanga sentensi ya tatu (Na.37) kwa kuandika herufi C na katika kuandika sentensi ya mwisho, watahiniwa 425,654 sawa na asilimia 45.38 walipanga sentensi ya nne (Na. 39) na kuandika herufi D kwa usahihi. Kiwango hiki cha kufaulu kwa watahiniwa katika kupanga sentensi hizo kinadhihirisha wazi kuwa, watahiniwa walikuwa na maarifa na uelewa wa kutosha kuhusu utungaji wa habari fupi zenye mantiki.

Kwa upande mwingine sehemu hii haikujibiwa vizuri na idadi ya watahiniwa 85,768 sawa na asilimia 9.16. Watahiniwa hao waliandika majibu kinyume na maelekezo ya swali kwa kujaza kipengele E ambacho hakikuwepo katika swali. Uchaguzi huo unaonesha kuwa, watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kufuata maelekezo ya swali kwa kupanga herufi toka A hadi D katika mtiririko sahihi.

## 2.5 Sehemu E: Ufahamu

Katika sehemu hii, watahiniwa walitakiwa kusoma kwa makini kifungu cha habari na kuandika jibu sahihi kutokana na habari hiyo. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa watahiniwa.


> Siku moja njiwa wawili walikwenda kunywa maji baada ya kula nafaka. Walipomaliza kunywa maji, mara alitokea samaki mmoja akawakaribisha na kusema, “Karibuni, hapa ndipo nyumbani kwangu. Siku zote mimi huishi kwenye maji.” Wale njiwa walimjibu, “Tunashukuru, lakini sisi tunaishi kwenye viota”. Njiwa mmoja alimuuliza samaki kama anaweza kuishi kwenye kiota. Samaki alijibu,“La hasha! Mimi ni kwenye maji tu.” Basi tangu hapo njiwa wakawa wamepata rafiki.
>
> Njiwa walikwenda tena kunywa maji siku nyingine. Walimkuta samaki anatapatapa majini, anavuta hewa kwa taabu. Samaki alipowaona aliwaambia, “Naomba mnipeleke kwenye mto mwingine wenye maji mengi, haya yanakauka, naangamia.” Wale njiwa wakamwambia, “Tunakuonea huruma lakini hatuna uwezo wa kukubeba.” Hata hivyo, “Wewe ni rafiki yetu, hatutakuacha ufe.” Samaki akajawa na matumaini. Wale njiwa walijadiliana bila kupata jibu.
>
> Baadaye samaki akapata wazo, akawaambia wale njiwa wachukue kamba moja fupi. Mmoja aing’ate huku na mwingine huku kwa kutumia midomo yao. Yeye angeuma katikati ile kamba. Halafu wale njiwa waruke na kumpeleka kwenye mto mwingine. Njiwa walifanya hivyo. Walitafuta kamba na baadaye wakaja kumchukua rafiki yao. Njiwa wale waliruka juu sana wakipita milima, mabonde na misitu.

Walipokuwa, juu ya msitu mmoja mnene, walikutana na ndege anayeitwa Korongo. Huyo aliwasifu wale njiwa kwa akili waliyotumia kumbeba yule samaki. “Loo! nyinyi njiwa mna akili sana!” Wale njiwa hawakujibu kwa sababu midomo yao ilikuwa, imeshikilia kamba. Rafiki yao samaki alifadhaika sana. Hakupenda njiwa wapate sifa wakati wazo alilitoa yeye.

Hakuvumilia, akataka kumwambia Korongo, “Ni mimi niliyewaelekeza.” Alipotaka kuzungumza, mdomo wake uliiachia ile kamba. Akaanza kudondoka kwenda chini. Wale njiwa walijaribu kumsaidia, wakashindwa samaki akafa. Kilichomponza samaki ni kutaka kwake sifa. Ama kweli sifa inaua.

**Swali la 41:** Kutokana na habari uliyoisoma, mwandishi anasema maisha ya samaki hutegemea nini?


Swali hili lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lilikuwa na lengo la kupima uwezo wa mtahiniwa katika kusoma habari kwa makini na kwa ufahamu. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 813,846 sawa na asilimia 86.78 waliweza kujibu swali hili vizuri kwa kueleza maisha ya samaki yanategemea maji. **Kielelezo 2.20** kinaonesha takwimu za kufaulu katika swali hili.




**Kielelezo 2.20:** *kinaonesha takwimu za kiwango cha kufaulu ambapo 86.78% ya watahiniwa waliweza kueleza kuwa, maisha ya samaki yanategemea maji.*

Uchambuzi zaidi katika skripti za watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa walioweza kujibu swali hili kwa usahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kwani walieleza kuwa, maisha ya samaki hutegemea maji. **Kielelezo 2.21** kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kutoa jibu linaloendana na matakwa ya swali.

**Kielelezo 2.21**



41. Kutokana na habari uliyoisoma, mwandishi anasema maisha ya samaki hutegemea nini?

Kutokana na habari uliyoisoma mwandishi anasema maisha ya sam-aki hutegemea maji.

**Kielelezo 2.21**: kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutumia kifungu cha habari kujibu swali kwa usahihi.

Aidha, watahiniwa 123,927 sawa na asilimia 13.2 walishindwa kueleza maisha ya samaki yanategemea nini kutokana na habari waliyosoma. **Kielelezo 2.22** kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali.

**Kielelezo 2.22**



41. Kutokana na habari uliyoisoma, mwandishi anasema maisha ya samaki hutegemea nini?

akataka Kumwambia korongo Tunakuonea huruma lakini hatuna uwezo wa kukubeba

**Kielelezo 2.22:** kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza maisha ya samaki yanategemea nini.

**Swali la 42:** Wazo la kumbeba samaki na kamba lilitolewa na nani?


Swali hili lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lilikuwa na lengo la kupima uwezo wa mtahiniwa katika kusoma habari kwa makini na kwa ufahamu. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 798,092 sawa na asilimia 85.10 waliweza kujibu swali hili vizuri. **Kielelezo 2.23** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa.




**Kielelezo 2.23:** *kinaonesha takwimu za kiwango cha kufaulu ambapo 85.10% ya watahiniwa waliweza kutoa jibu sahihi.*

Takwimu zaidi za kufaulu zinaonesha kuwa, watahiniwa wengi waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kutaja mhusika aliyetoa wazo la kumbeba samaki kwa kamba kuwa, ni “*samaki”.* **Kielelezo 2.24** kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kutoa jibu linaloendana na matakwa ya swali

**Kielelezo 2.24**



42. Wazo la kumbeba samaki na kamba lilitolewa na nani?

Wazo la kumbeba samaki na kamba lilitolewa na samaki.

**Kielelezo 2.24:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutaja mhusika aliyetoa wazo la kumbeba samaki.

Jumla ya watahiniwa 139,746 sawa na asilimia 14.9 hawakuweza kujibu swali vizuri kwani walishindwa kumbaini aliyetoa wazo la kumbeba samaki. **Kielelezo 2.25** kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.

**Kielelezo 2.25**



42. Wazo la kumbeba samaki na kamba lilitolewa na nani?

njiwa walijaribu kamsaidia wakashindwa samaki akafa

**Kielelezo 2.25:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa jibu sahihi.

**Swali la 43:** Unafikiri kwa nini njiwa hawakumjibu Korongo?”


Swali hili lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lilikuwa na lengo la kupima uwezo wa mtahiniwa katika kusoma habari kwa makini na kwa ufahamu. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 783,110 sawa na asilimia 83.50 walijibu swali hili vizuri. **Kielelezo 2.26** kinaonesha takwimu za majibu ya watahiniwa.




**Kielelezo 2.26:** *kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo 83.50% ya watahiniwa waliweza kutoa sababu za njiwa kutokumjibu korongo.*

Uchambuzi zaidi wa skripti za watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kwani waliweza kusoma kifungu cha habari na kueleza sababu ya njiwa kukataa kumjibu korongo. **Kielelezo 2.27** kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili.

**Kielelezo 2.27**



43. Unafikiri kwa nini njiwa hawakumjibu Korongo?

Njiwa hawakumjibu Korongo kwa sababu midomo yao ilikuwa imeshi-kilia kamba.

**Kielelezo 2.27:** Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali kwa usahihi.

Aidha, watahiniwa 154,731 sawa na asilimia16.5 walishindwa kueleza sababu ya njiwa kukaa kimya kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kutosha kubaini maudhui yaliyomo katika kifungu cha habari **Kielelezo 2.28** kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

**Kielelezo 2.28**


43. Unafikiri kwa nini njiwa hawakumjibu Korongo?


HUYU ALIWASIFU NJIWA KWA HAKILI WAUYOTUMIA KUMBEBA SAMAKI

**Kielelezo 2.28:** *kinaonesha* sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

**Swali la 44:** Andika kichwa kinachofaa kwa habari uliyoisoma.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lilikuwa na lengo la kupima uwezo wa mtahiniwa kutambua kichwa cha habari.


Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 516,906 sawa na asilimia 55.1 waliweza kubaini kichwa cha habari. **Kielelezo 2.29** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa.




**Kielelezo 2.29**:kinaonesha *kiwango cha kufaulu ambapo 55.12% ya watahiniwa waliweza kuandika kichwa cha habari "samaki aliyependa sifa".*

Uchambuzi zaidi wa skripti za watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa walioweza kubaini kichwa cha habari ambacho ni "urafiki wa samaki na njiwa" walikuwa na uwezo wa kusoma na kuelewa maudhui ya kifungu cha habari. **Kielelezo 2.30** kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili.

**Kielelezo 2.30**



44. Andika kichwa kinachofaa kwa habari uliyoisoma?
URAFIKI WA SAMAKI NA NJIWA.

**Kielelezo 2.30:** *kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika kichwa cha habari kinachofaa kutokana na habari aliyosoma.*

Aidha, watahiniwa 420,939 sawa na asilimia 44.9 walishindwa kuandika kichwa cha habari kinachofaa kulingana na habari waliyosoma kwa kushindwa kuelewa maudhui ya kifungu cha

habari. **Kielelezo 2.31** kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

**Kielelezo 2.31**



44. Andika kichwa kinachofaa kwa habari uliyoisoma?

njiwa wawili walikwenda kunywa maji baada ya kula nafaka

**Kielelezo 2.31:** *kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kichwa cha habari.*

**Swali la 45:** Andika funzo ulilolipata kutokana na tabia ya samaki.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lilikuwa na lengo la kupima uwezo wa mtahiniwa katika kusoma habari kwa makini na kuelezea funzo linalopatikana. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu ambapo watahiniwa 502,384 sawa na asilimia 53.6 walishindwa kueleza funzo linalopatikana katika kifungu cha habari kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kubaini maudhui ya kifungu cha habari **Kielelezo 2.32** kinaonesha takwimu za majibu ya watahiniwa.



**Kielelezo 2.32:** *kinaonesha* takwimu za ki*wango cha kufaulu ambapo 53.57% ya watahiniwa walishindwa kujibu swali hili.*

Uchambuzi zaidi wa skripti za watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa hao walishindwa kubaini funzo kutoka katika kifungu cha habari. **Kielelezo 2.33** kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 2.33**

45. Andika funzo ulilolipata kutokana na tabia ya samaki?

WEWE NI RAFIKI YETU HATU TAKUACHA UFE.

**Kielelezo 2.33:**kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

Aidha, watahiniwa 435,371 sawa na asilimia 46.4 waliweza kubaini funzo linalopatikana katika kifungu cha habari ambalo ni “Sifa zinaua ”kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuelewa maudhui ya kifungu cha habari **Kielelezo 2.34** kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali kwa usahihi.

**Kielelezo 2.34**

45. Andika funzo ulilolipata kutokana na tabia ya samaki?

Kutokana na tabia ya samaki funzo nililolipata ni kutokupenda sifa.

**Kielelezo 2.34:** kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutoa funzo linalopatikana kutokana na tabia ya samaki.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI

Mada zilizotahiniwa katika somo la Kiswahili ni *Sarufi*, *Lugha ya Kifasihi*, *Ushairi, Utungaji na Ufahamu*. Uchambuzi unaonesha kuwa, kiwango cha kufaulu ni kizuri katika mada ya *Ufahamu* (71.38%) na *Lugha ya Kifasihi* (70.89%). Kiwango cha kufaulu ni cha wastani katika mada ya *Ushairi* (58.81%), *Utungaji* (57.14%) na *Sarufi* (57.07%). Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi na watahiniwa katika mada ya *Sarufi* ni swali la 4 (88.44%), 20 (79.01%), 6 (74.94%) 16 (72.37). na la 19 (71.05). Katika mada ya *Lugha ya Kifasihi*, swali la 24 (85.67%), 21 (83.90%), 26 (83.15%), 22 (81.86%). na la 23 (80.10%). Aidha, katika mada ya *Ushairi* swali la 33 (76.96%), 31 (74.33%) na la 34 (74.12%) ni kati ya maswali yaliyojibiwa vizuri. Mada ya *Utungaji* ilikuwa, na maswali mawili yaliyojibiwa vizuri ambayo ni swali la 40 (74.63%) na la 38 (61.78%). Katika mada ya *Ufahamu* swali la 41 (86.78%), 42 (85.10%) na la 43 (83.50%) yalikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu. Hata hivyo, swali lililojibiwa vizuri zaidi kuliko mengine ni swali la 4 (88.44%) kutoka katika mada ya *Sarufi*.

Aidha, yapo maswali yaliyokuwa na viwango hafifu vya kufaulu kutoka katika kila mada. Katika mada ya *Sarufi* swali la 2 (30.24%) na la 15 (31.00%) na katika mada ya *Lugha za Kifasihi* swali la 30 (29.42%) lilikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu. Aidha, katika mada ya *Ushairi* swali la 35 (20.51%) na 32 (36.97%) yalikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu ambapo swali la 35 (20.51%) lilikuwa na kiwango hafifu zaidi cha kufaulu.

Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa mada kati ya PSLE 2017 na 2018 kinaonesha kuna kiwango vya kupanda na kushuka kwa

mada mbalimbali. Uchambuzi unaonesha kuwa mwaka 2018 mada za *Lugha za Kifasihi* na *Ufahamu* zimekuwa, na ongezeko la viwango vya kufaulu ukilinganisha na mwaka 2017 kutoka asilimia 60.40 hadi kufikia asilimia 70.89 katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* sawa na ongezeko la asilimia 10.49 kwa mwaka 2018. Katika mada ya *Ufahamu*, kiwango cha kufaulu kimeongezeka kutoka asilimia 66.45 hadi 71.38 sawa na ongezeko la asilimia 04.93.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa mwaka 2018 kumekuwa na kiwango hafifu cha kufaulu ukilinganisha na mwaka 2017 kwenye mada ya *Sarufi, Ushairi* na *Utungaji.* Mada ya *Sarufi* wastani wa kufaulu umepungua kutoka asilimia 61.17 hadi 57.07 ambapo ni pungufu kwa asilimia 04.10. Hata hivyo mada ya *Ushairi* haikujibiwa vizuri katika mwaka 2018, kwani kumekuwa na kiwango pungufu cha kufaulu kutoka asilimia 67.75 hadi kufikia asilimia 58.81 sawa na pungufu ya asilimia 08.94. Aidha, katika mada ya *Utungaji,* wastani wa kufaulu umepungua kutoka asilimia 71.00 hadi 57.14 kwa upungufu wa asilimia 13.86 Uchambuzi wa viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa kila mada umewasilishwa katika **kiambatisho A na kiambatisho B.**

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa mada unaonesha kuwa, kiwango cha kufaulu kwa mada zote katika mwaka 2018 ni kizuri sawa na mwaka 2017 licha ya kuwa, kumekuwa na upungufu wa asilimia 2.29. Mwaka 2017 kiwango cha kufaulu kilikuwa asilimia 65.35 ukilinganisha na mwaka 2018 ambapo kilikuwa asilimia 63.06.

Hata hivyo, uchambuzi wa viwango vya watahiniwa walivyojibu maswali umebainisha dosari zilizowafanya watahiniwa washindwe

kujibu maswali kwa usahihi. Miongoni mwa dosari hizo ni kushindwa kutambua matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana za msamiati, vifungu vya maneno, ngeli za majina, visawe na mbinu za kusoma kwa ufahamu. Dosari nyingine ni kutokujibu kabisa baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo.

Ili kukabiliana na changamoto za ufundishaji na ujifunzaji, ni vema juhudi za makusudi zifanyike ili kuwawezesha watahiniwa kuwa na weledi wa kumudu somo la Kiswahili ambalo pia ni lugha ya Taifa na kielelezo cha utamaduni wa Mtanzania.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

(a) Walimu wanatakiwa kuweka msisitizo katika ufundishaji wa dhana za msamiati wa Kiswahili ili kuwajengea wanafunzi umahiri wa kubaini maana za msamiati.

(b) Walimu wawajengee wanafunzi misingi madhubuti ya kubaini aina za maneno kwa kuzingatia kanuni za kisarufi katika uundaji wa sentensi.

(c) Walimu wawaelekeze wanafunzi dhana ya upatanisho wa kisarufi ili kubaini umoja na wingi katika sentensi kwa kuzingatia ngeli za majina.

(d) Walimu wawahimize wanafunzi kushiriki katika mashindano mbalimbali ya uandishi wa insha yanayotumia lugha ya Kiswahili.

(e) Walimu wanatakiwa kuweka msisitizo katika ufundishaji wa mashairi kwa kuzingatia muundo wake ikiwa ni pamoja na maana ya msamiati wa kishairi

**KIAMBATISHO A**

## ULINGANIFU WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA KILA MADA KATIKA PSLE 2017 NA PSLE 2018

| Na | Mada | Mtihani wa 2017 | | | | Mtihani wa 2018 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu (%) | Maoni | Kufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | |
| 1. | Sarufi | 1 | 90.40 | 61.17 | Vizuri | 1 | 53.19 | 57.07 | Wastani |
| | | 2 | 52.60 | | | 2 | 30.24 | | |
| | | 3 | 36.40 | | | 3 | 54.27 | | |
| | | 4 | 48.00 | | | 4 | 88.44 | | |
| | | 5 | 73.40 | | | 5 | 51.05 | | |
| | | 6 | 77.90 | | | 6 | 74.94 | | |
| | | 7 | 30.30 | | | 7 | 45.34 | | |
| | | 8 | 23.60 | | | 8 | 52.94 | | |
| | | 9 | 78.40 | | | 9 | 55.28 | | |
| | | 10 | 80.10 | | | 10 | 52.46 | | |
| | | 11 | 73.30 | | | 11 | 66.30 | | |
| | | 12 | 66.80 | | | 12 | 45.71 | | |
| | | 13 | 70.00 | | | 13 | 62.74 | | |
| | | 14 | 52.00 | | | 14 | 46.09 | | |
| | | 15 | 69.90 | | | 15 | 31.00 | | |
| | | 16 | 62.90 | | | 16 | 72.37 | | |
| | | 17 | 81.70 | | | 17 | 48.32 | | |
| | | 18 | 44.60 | | | 18 | 60.79 | | |
| | | 19 | 88.70 | | | 19 | 71.05 | | |
| | | 20 | 25.40 | | | 20 | 79.01 | | |
| 2. | Lugha ya Kifasihi | 21 | 70.40 | 60.40 | Vizuri | 21 | 83.90 | 70.89 | Vizuri |
| | | 22 | 57.10 | | | 22 | 81.86 | | |
| | | 23 | 52.70 | | | 23 | 80.10 | | |
| | | 24 | 14.40 | | | 24 | 85.67 | | |
| | | 25 | 69.20 | | | 25 | 71.56 | | |
| | | 26 | 49.30 | | | 26 | 83.15 | | |
| | | 27 | 80.90 | | | 27 | 73.69 | | |
| | | 28 | 89.70 | | | 28 | 74.33 | | |
| | | 29 | 68.90 | | | 29 | 45.23 | | |
| | | 30 | 51.40 | | | 30 | 29.42 | | |
| 3. | Ushairi | 41 | 71.40 | 67.75 | Vizuri | 31 | 74.33 | 58.81 | Wastani |
| | | 42 | 80.40 | | | 32 | 36.97 | | |
| | | 43 | 68.90 | | | 33 | 76.96 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 44 | 77.30 | | | 34 | 74.12 | | |
| | | 45 | 71.60 | | | 35 | 20.51 | | |
| | | 46 | 36.90 | | | 36 | 69.99 | | |
| | | 41 | 71.40 | | | | | | |
| | | 42 | 80.40 | | | | | | |
| | | 43 | 68.90 | | | | | | |
| | | 44 | 77.30 | | | | | | |
| 4. | Utungaji | 47 | 72.30 | 71.00 | Vizuri | 37 | 46.77 | 57.14 | Wastani |
| | | 48 | 72.00 | | | 38 | 61.78 | | |
| | | 49 | 68.00 | | | 39 | 45.38 | | |
| | | 50 | 72.70 | | | 40 | 74.63 | | |
| 5. | Ufahamu | 31 | 82.90 | 66.45 | Vizuri | 41 | 86.78 | 71.38 | Vizuri |
| | | 32 | 85.90 | | | 42 | 85.10 | | |
| | | 33 | 67.00 | | | 43 | 83.50 | | |
| | | 34 | 56.50 | | | 44 | 55.12 | | |
| | | 35 | 49.60 | | | 45 | 46.42 | | |
| | | 36 | 85.90 | | | | | | |
| | | 37 | 44.30 | | | | | | |
| | | 38 | 68.40 | | | | | | |
| | | 39 | 63.40 | | | | | | |
| | | 40 | 60.20 | | | | | | |

## KIAMBATISHO B

